

22H-Maddul-Far-'iy (Matawi)

المَدُّ الْفَرْعِيّ - Al-Maddul-Far-'iy (Matawi):

Madd ambayo hutegemea sababu nyengine ima iwe hamzah au sukuwn ili iweze kurefushwa kuvutwa kwake kuishinda مَدُّ الطَّبِيعِيّ (maddutw-twabiy'iy) na hiyo sababu ya nje. Imeitwa 'Al-Far-iy' (tawi) kwa sababu madd hizi sio za asili bali zimechipuka kutoka katika مَدُّ الطَّبِيعِيّ (maddutw-twabiy'iy).

مَدُّ الْفَرْعِيّ Maddul-Far-'iy Hugawanyika sehemu mbili kutokana na sababu inayopelekea kuwa madd:

- Madd kutokana na hamzah

- مَدُّ الْوَاجِبِ الْمُتَّصِلِ Maddul-Waajib Al-Muttaswil
- مَدُّ الْجَائِزِ الْمُتَفَصِّلِ Maddul-Jaaiz Al-Munfaswil
- مَدُّ الصَّلَاةِ الْكُبْرَى Maddusw-Swillatil-Kubraa

- Madd kutokana na sukuwn

- مَدُّ الْعَارِضِ لِلْسُّكُونِ Maddul-'aaridhwi lis-sukuwn
- مَدُّ اللَّيْنِ Maddul-liyn
- مَدُّ الْإِلْزَامِ Maddul-laazim